

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM ANATOA
MWALIKO KWA WAFANYABIASHARA WAKUBWA KWA WADOGO
KUWASILISHA MAOMBI YA KUSIMAMIA NA KUENDESHA VIOSKI VYA
VYAKULA VYA ASILI NA VINYWAJI KATIKA ENEO LA UFUKWE WA
BARACK OBAMA KARIBU NA HOSPITALI YA AGA-KHAN KWA LENGU LA
KUVUTIA WATALII WA NJE NA NDANI YA NCHI**

MWALIKO WA MAOMBI YA KAZI ZA HUDUMA

- 1.** Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeandaa eneo la utalii wa vyakula vya asili na vinywaji katika eneo la ufukweni wa Barack Obama linalojulikana kama “Forodhani in Dar” kwa kuzingatia hivyo Halmashauri inatarajia kupata mapato kutokana na chanzo hiki cha mapato kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Halmashauri ya Jiji inatarajia kuwapata watoa huduma wa vioski viwili na wafanyabiashara wadogo wadogo watakaotoa huduma za vyakula vya asili na vinywaji kwa kutumia meza ndogo kwenye eneo lenye ukubwa wa mita sita (6) za mraba kwa kila mfanyabiashara katika eneo la ufukwe wa Barack Obama uliopo karibu na hospitali ya AGA-KHAN

2. Waombaji wanakaribishwa kuwasilisha maombi yao **Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam**, yakionyesha anataka kufanya biashara gani maombi yote yaandikwe kwa usahihi na yafungwe kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa jina la kazi mojawapo tajwa hapa chini:

- i. **Kusimamia na kuendesha vioski vya vyakula vya asili na vinjwaji katika eneo la ufukwe wa Barack Obama “Forodhani in Dar” uliopo karibu na hospitali ya AGA-KHAN**
- ii. **Kazi ya huduma ya vyakula vya asili kwa kutumia meza na miavuli.**

Maombi haya ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam S.L.P. 9084, Dar es Salaam Kitengo cha Manunuzi (PMU).

3. **Waombaji wa vioski wanatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-**

- a) Waombaji wanatakiwa wawe na viti na miavuli kwa ajili ya wateja
- b) Waombaji wanatakiwa wawe na uwezo wa kupika vyakula vya asili vya Kitzania pamoja na vyakula vinavyopendwa na wageni
- c) Waombaji wanatakiwa wawe na Leseni ya Biashara
- d) Waombaji wanatakiwa kuonyesha kiasi watakachowasilisha Halmashauri ya Jiji Kama gharama za kupangishwa makontena yaliyopo katika eneo hilo. Bei zinapaswa kutolewa katika Shilingi za Kitzania.
- e) Kiwango kilichotajwa na mtoa huduma kiwe kimekamilika na hakitabadilika katika kipindi chote cha mkataba na hakitaingizwa kwenye marekebisho kwa sababu yoyote ile.
- f) Waombaji wanatakiwa kuwa tayari kulinda eneo na mali zake pamoja na kutunza mazingira ya eneo hilo.
- g) Mwombaji anatakiwa kuwa tayari kulipa dhamana ya huduma hii ambayo ni fedha ya **miezi mitatu (3)** yenye thamani sawa na kiasi

alichoomba kulipa kwa mwezi ambayo itakuwa ni dhamana ya zabuni hii. Fedha iliyoshikiliwa itatolewa baada ya kumalizika kwa mkataba.

h) Waombaji watakuwa wanatoa huduma masaa ishirini na nne (24).

4. Waombaji wa biashara ndogo ndogo watakaouza kwa kutumia meza na miavuli wanatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- a. Waombaji wataanza kutoa huduma kuanzia saa sita (6) mchana hadi saa tano (5) usiku.
- b. Waombaji wanatakiwa kuwa tayari kulinda eneo na mali zake pamoja na kutunza mazingira ya eneo hilo.
- c. Waombaji wanatakiwa kuwasilisha barua ya utambulisho kutoka Serikali yake ya Mtaa.
- d. Waombaji wanatakiwa kuonyesha kiasi watakachowasilisha Halmashauri ya Jiji kama gharama za kupangisha eneo la kuweka meza za biashara.
- e. Waombaji waonyeshe wanatarajia kutoa huduma gani kwa mfano kuuza urojo, mihogo ya kukaanga, kande, ugali, kishumba, mlenda n.k.

Waombaji wote wanakaribishwa kutembelea eneo la Ufukwe wa Barack Obama karibu na Hospitali ya Agha-Khan kwa ajili ya kujiridhisha kabla hajawasilisha maombi yake.

Mwombaji anatakiwa kuwa tayari kulipia gharama za taka ngumu kwa mujibu wa sheria ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, hivyo ni lazima awe na vifaa vya kutupia taka na utaratibu wa kudhibiti maji taka yatakayotumika katika shughuli atakayokuwa anafanya.

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni *Jumatatu tarehe 15 Juni, 2020 saa 8:00 Mchana.* Maombi yote yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa

waombaji walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi wa maombi katika ***Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji*** la Dar es Salaam S.L.P. 9084, Dar es Salaam Kitengo cha Manunuzi (PMU).

6. Maombi yatayochelewa, sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi yasiyofunguliwa katika tukio la ufunguaji maombi, kwa hali yoyote ile maombi hayo hayatakubaliwa kwa tathmini.

Sipora J. Liana

**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**